

Msimulizi, 1888¹

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The periodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1889.

In an earlier BARUA YA KUELEZEA KWA ndugu zetu Wamasihya wakaao katika killa mji wa Upelekwa wetu (Universities' Mission to Central Africa) Salaam sana. Sisi hapa waalimu wa Kiungani tunawaarifu kama tumefanya shauri tukisayidiwa na Kasisi yetu hapa. Na shauri lenyewe kubwa, tunawataka mwe rathi mkatusayidie shauri letu liendelee sana. Tunaambiwa kama katika killa Chuoni kubwa kule Uingereza watoto wa Chuoni huandika habari za Chuoni yao marra kwa marra na kuzipiga chapa kufanya kama kitabu kidogo, huitwa Kiingereza "School Magazine," bassi huzipiga chapa katika killa mwezi ao marra sita kwa mwaka, huzipeleka hizi "Magazines" kwa

¹ The text is issued under licence CC BY-NC

wakubwa wao waliokaa zamani Chuoni, wapendao, hatta wakiwa wametoka, kusikia habari kama kule Chuoni watu hawajambo na kuendelea. Bassi na wale wanaosoma bado Chuoni hupenda pia kuzipata habari zao wale watu wazima waliokaa Chuoni zamani, hatta huwaambia waandike habari za killa mji wanapokaa na habari za kazi wanazozitenda wakazilete kwao watoto wa Chuoni zipate kupigwa chapa marra kwa marra katika vile vitabu viitwavyo "Magazines."

Bassi kwa kufanya hivi killa mtu akisoma vitabu hivi anavyoletewa marra kwa marra hupata habari sawasawa za wale wenziwe wa zamani aliocheza nao waliposoma pamoja zamani Chuoni; hatta wakiwa wanakaa mbali sana huweza kama kusimuliana habari zao, kwa kuzisoma katika vitabu hivi marra kwa marra. Ndivyo watendavyo watu wengi sana kule Uingreza. Bassi na sisi hapa tumepata kufanya shauri ya kutenda vile vile. Kwani hapa Kiungani tukiisha kukaa siku nyingi tunatawanyika huko na huko, killa mtu kwa kazi yake, tukikaa mbalimbali sana, tukijaribu kufanya kazi zile

MSIMULIZI. 4

KUJA KWAKE SAYID KHALIFA KIUNGANI.

SIKU ya Bartolomayo hii ilikuwa siku ya furaha huku Unguja. Watoto wa Mkunazini, na wa Mbweni wakaja hapa Kiungani kufanya siku kuu. Walakini siku haswa ya Bartolomayo ilikuwa Aug. 24, siku ya Jumaa, bassi kwa sababu hii hatukufanya karamu tulipamba tu siku hii, na Juma a mosi ikawa mahali pake. Watu wa manowari wakatuazima bandera nyingi sana tukazitunga tangu mnazi hatta mnazi nje, na nyumbani pia. Assubui na mapema kiisha kutoka kanisani tukatengeneza uwani, na tukalima mahali vizuri pa kuwekea gari la farasi la Sayid, kwani tukasikia kama Sayid Khalifa Mfalme wa Unguja amekubali kuja kututazama. Tulipokwisha tukacheza mpaka athuuri, tukaenda Chuoni kununua zawadi pamoja na Wamjini, na Wambweni, na sisi wa Kiungani, kiisha tukacheza hatta saa kumi. Akafika Balyozi mkubwa na Admeli Mwingreza na Wazungu wengi sana, hatta halafu tukasikia yakuwa Sayid anakuja, wote tuliokuwapo siku hiyo tukaenda barazani kumlaki na kumsalimia, lakini kwanza akapitia kwa njia ya pwani ndogo gari lake likakwamakwama, akarudi ukapitia njia kuu, akatufikia na askari zake nyuma, alipofika tukamwamkia hivi; Hip! Hip! Hip! Hurrah! Hurrah! marra tatu, akashuka garini akaenda sebuleni ya ndani, na Waalimu wakaenda kusimama sebule ya nje.

Alimopita tu kwanza mmetiwa nguo nyekundu iliotoka kwa Balyozi, alipokuwa kule sebuleni akaletewa kahawa na shalhati, kiisha akaenda Chumba cha kupigia Chapa, akapewa karatasi zikaenda pigwa chapa, maneno ya Kiarabu ya kumshukuru kwa urathi wake kwetu, akapiga moja mwenyewe, kiisha, akatoka watu wakipiga, Hip! Hip! Hip! Hurrah! kiisha akaenda sebuleni na watoto wakaenda barazani, kiisha akatoka sebuleni akaingia garini mwake, watu wakapiga kelele ya kumwaga; Hip! Hip! Hip! Hurrah!

MSIMULIZI. 5

akaenda zake, halafu na sisi tukagawanyika killa mtu kwake.

Na siku hii tulikarimiwa sana, Sayid alileta Rs 200 zigawanyike kwa watoto wa Mission, na Balyozi Rs 50, la Balyozi mdogo Rs 20, na Mzungu mmoja akatoa Rs 90 na mwingine Rs 10. Zile 200, tukanunuliwa zawadi, na zile 50 tukagawiwa killa mtu sawa-sawa na zile 20 tunakwenda nazo kushinda mahali, na zile Rs 90 zimepelekwa Ulaya kwenda kununua michezo ya kuchezea. Mzungu mwenyi Rs 90 hakutaka jina lake lijulikane, kwa sababu hiyo hatulijui jina lake, zile Rs 50 tumepewa killa mtu pesa kumi kumi, wa Mjini, wa Mbweni, na sisi wa hapa Kiungani. Mtg.

HABARI ZA PWANI YA BARA.

SIKU hizi habari za miji ya pwani zimechafuka sana tangu Tanga hatta Lindi na Mikandani. Labda Wadoicha wamekosa utaratibu katika kuanza shughuli yao ya biashara, hatta wamethaniwa wanakuja kutwaa inchi ya watu wa pwani. Bassi katika Tanga ukatokea ugomvi na manowari ya Wadoicha wakapiga mzinga wakateketeza mji. Kule Bagamoyo waliua watu 105 waliotaka kuvunja nyumba ya Wadoicha kule na kuwaharibu wenyewe; kule Kilwa Wadoicha wawili wafanya biashara mmoja ameuawa, mmoja amejiua. Lakini Pangani haswa ndio uthia mwingi; Waswahili wamewakasirikia sana Wadoicha, hatta haujaisha bado hatta kidogo. Tuliona hofu kama labda watawatwalia kisasi ndugu zetu wa Boonde wakiwaona sawa na Wadoicha, lakini mmoja wa wakubwa wa vita Pangani ameandika hivi kwa Balyozi Mwingreza. "Baada ya salaam ujue, wewe rafiki yetu, kama sisi hapa na watu wako kule Magila hatuna ugomvi, Hatujaona ubaya kwao wala hawajaona ubaya kwetu. Nao watu wako wamekuwa kama watu wetu. Hapana

MSIMULIZI. 6

sababu wahame wakaende Unguja, lakini ukipenda tutapeleka watu wetu kwenda Magila kuwatwaa, wakitaka kuja wenyewe, watafuatana nao. Tutawapakia chomboni kuwaleta kwako. Hapana lazima kuleta manowari. Wakitaka wenyewe kukaa kwao tutawaacha. Watu wote Waingereza, Wahindi, Wabanyani, usiwaonee hofu. Tangu zamani hapana ugomvi nao. Lakini tunagombana na Wadoicha kwa sababu wanataka kutwaa ufalme wetu."

GINSI TULIVYOWAAGA NDUGU ZETU KWENDA NYASSA.

Katika siku ya Jumaa Aug. 10 ilikuwa siku ya kuwaaga ndugu zetu tuliyo wasafirisha kwenda Nyassa wamfanyie Muungu kazi, na twalikusanyika kuwafanyia mwagano, Wazungu wote wa hapa Kiungani, na sisi watoto wa hapa, na bibi wa Mbweni, Miss Berkeley, na waanawake wawili wa Mbweni, Monika Hurumanani na Emma Nyawela, na assubui saa ya kwanza Jumaa palikuwa na Usharika Mtakatifu kwao hao ndugu zetu wanne Augustine Ambali, Denys Sayite, William E. Kanyopolea, na Leonard Pesa. Hatta tulipokwisha sala ya Usharika, ikawa kuwasayidia ndugu zetu kufunganya mizigo yao. Jioni ilikuwa sala kwao wasafiri, killa mmoja walikaa kanisani katika viti mbele ya mathbahu, wamevaa "Cassock" na "Surplice" kwanza tukasema sala ya jioni kidogo, tena tukaimba wimbo wa mwagano, tena pakawa na mahubiri kwao wasafirio, na mwenyi kuwahubiria ndiye Mr Jonea-Bateman; na maneno aliyoyatoa kwao yalikuwa maneno ya kuwatia moyo kama wasione hofu na kuchoka katika kazi yao illa wawe imara, hatta wakiwa wachache, lakini waishike tu kazi yao; na tena kasisi wetu katika kuwaambia maneno ya mwisho, aliwaambia, Ndugu zangu, Msiogope-enyi kikundi kidogo; kwani Bwana wetu alisema kwa Mitume mbele ya kupaa kwake mbinguni, alisema,

MSIMULIZI. 7

Enendeni, wafundisheni mataifa yote, mwabatize kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, mwafundishe washike yote niliyowaamuru: nami nipo pamoja nanyi siku zote, hatta mwisho wa dunia. Bassi naye asema kwenu leo, nanyi msiogope, enyi kikundi kidogo, kwani mkitenda kazi zenu yee yupo pamoja nanyi.

Tena alipokwisha kuhubiri killa mmoja akapokea mbaraka. Tena tukaimba wimbo wa 148, tena sala kidogo, halafu sala ya jioni ikaisha.

Tukaingia mezani na tulipokuwa mezani, akatokea mwalimu Augustine akatuaga wote kwa sauti ya kusikiwa, akasema, Nitapenda mno kusikia habari za killa mtoto kama zitakuwa njema, juu yote msisahau kutuombea, kwani sala zenu zinahitajiwa mno. William E. Kanyopolea akatokea mezani, na killa mtu amesimama mahali pake, akasema, Kuaherini mno, bali baada ya kuaheri, nasema juu yenu waalimu kwanza, kama msilegee katika kuwatunza watoto hawa, wala sisemi kama sisi ndio tumewatunza watoto, na pasipo sisi hamwezi kuwaangalia, hashu, illa kama Muungu alivyotujalia wote kuwa juu yao watoto wote, kwa hiyo tumwombe yee atatupa nguvu za kutenda killa jambo, naswi tunaenda zetu mbali illa tunapenda kusikia vilevile kama mnazidi kuendelea mbele. Nanyi watoto mwatii waalimu wenu; wala msiseme, Oh! akina fulani wameondoka nitafanya hivi na hivi, haifai. Tena akatuaga wote akatoka.

Akatoka mwalimu Denys Sayite akasema, Ninyi waalimu angalieni sana mkimwona mmoja wa watoto wetu akifanya neno lolote mkatazeni, msimwache; kwani mkimwacha, ni juu yenu, bassi angalieni roho zao zi mkononi mwenu, nanyi hamwezi kuwaangalia wao, msipojiangalia ninyi wenyewe; kwani hawa watoto hawana buddi kufuatisha namna zenu. Na tena nyie nyote angalieni tunawaambieni na mapema, kama barua zenu twazihitaji mno, mtueleze habari zote za nyumba, bali marufuku kwa mtoto wowote

MSIMULIZI. 8

kutia ndani ya barua kosa la mtu mwingine, hatutaki jambo kama hilo, kwani killa mtu ni mkosaji, na tukipata barua yoyote ya mtoto iliyoandikwa ndani yake kosa la mwenziwe, kurudisha tutamrudishia mwenyewe. Watoto mwatii waalimu wenu, myatii yote na amri za nyumba, mshike yote mnayoambiwa, mwasikie killa neno wawaambialo, na juu yote waalimu mwangalie sana kondoo hawa wasipotee, angalieni ni juu yenu wakipoteta. Bassi angalieni, ndugu, imewapasa ninyi wenyewe kwanza mwe hodari msichoke, shauri lenu liwe moja tu. Naswi twawaaga leo tunaenda zetu tunatumaini kusikia habari za killa mtu. Tena akaja Mr Goodyear akasema, Nawashukuru sana waalimu kwani mmenisayidia sana, na juu yote bado siku chache naenda zangu Magila, niombeeni nifike salama. Na katika hao ndugu zetu, pana mmoja naye amekwenda Nyassa pamoja nao, jina lake Aruffo Tangani, mpishi, naye ana mke wake; tena Augustine ana mke wake. Bassi Augustine, William Edward na Denys na Aruffo wakaja wakawaaga watoto wote wangine, na wangine tukawasindikiza hatta bandarini: na Mr Clarke na Mr Jones-Bateman wakawasindikiza hatta merikebuni, na sisi wote tuliofuatana nao walipotuaga hapo pwani, tukajirudia zetu, tukawasili nyumbani, tukaenda lala.

Hatta saa thenashara assubui Juma amosi Aug. 11 meli ikang'oa nanga, ikaenda zake. Na bado siku tatu akasafiri naye Leonard Pesa kwenda Magila. H.S.M.

(Tumepata barua zao zinazotoka Vincenti katika mto Shire, wakisema wamefika salama karibu na Blantyre.) Mtg.

Zamani alisoma hapa Kiungani mtoto, jina lake Henry Wright Duta, Mganda, lakini alikuwa ameisha rudi Uganda zilipotokea zile taabu kuu kwa ndugu zetu Wamasihya wa

MSIMULIZI 9

kule, wakiteswa na kufukuzwa na Mfalme wao. Bassi na yeye pia walimtafuta wamuue, lakini halafu uthia ukitulia waliweza kuonekana tena. Hatta mwaka huu nimepokea barua hii kwake. Inaonyesha sana ginsi walivyoongezeka Wamasihiya kwa taabu zile zilizowapata, na kama Waganda walipewa neema kustahimili vema mafukuzo.

Natete, Buganda, Nov. 15, 1887.

"My dear Mr. Bateman,

Salaamu sana, baada ya salaam, Sasa hapa tumepata amani kidogo, labuda mimi nakumbuka umepata kusikia habari zile za shidda ilitupata katika May, 1886. Twaliuthika sana sana, ndugu yangu, katika hatari ilitupata, twalikuwa tukiomba msituni na tukisoma msituni, siku nyingi sana, lakini sasa siku hizi tunaweza kukusanyika kanisani kuomba, na kusikia kukhutubu, hatta mimi sasa nimepewa ruhusa kukhutubu kuhubiri habari ya Isa, Wazungu wakaniambia, kwani ndio kazi yako, bassi na mimi sina buddi kujifunza kazi hii, siku hizi watu wamekuwa wengi kuliko kwanza, katika shidda hii watu wamedumu sana sana kushika habari ya Isa na maneno yake, sasa tuwajua wenyi kushika wapata aroba mia, naona sisi tumebarikiwa sana katika inchi yetu kupita inchi za washenzi wenzetu. Waganda wapenda sana kusikia na kutaka kujua habari za Isa, na kushika upesi, kama si hivyo hawangalikuja marra ya pili kusoma, kwa shidda hii iliyotupata, lakini wao wamezidi kuja killa siku, na katika wale waliokamatwa settini, hatta mmoja aliyekana kusema kwamba mimi Isa simjui, lakini hawa wote, wakaungama kwamba sisi tumemwamini Isa ndiye Mwana wa Muungu tumekubali kufa kwa ajili yake, kwani aweza yeye kutufanya hayi.

Bassi hawa wote watu settini. Wakatwaliwa wakachomwa moto, wakafa kwa ajili ya Ufufuo wake Isa. Mimi rafiki yako akupendaye dayima katika Bwana, Henby Wright Duta."

MSIMULIZI. 10

Na mwezi huu tumesikia habari za Uganda, kama moyo wa Mfalme yule Mwanga umegeuka sana, anawakaribisha kwa heshima sana Wazungu wale waliokwenda kufundisha ndugu zetu za huko. Labda naye siku moja ataongoka mwenyewe. P.L.J-B.

HABARI ZA MBWENI.

Jumaa Oct. 5 lilikuwa kusanyiko la Chama ya Mchungaji mwema wa Waalimu wa Mbweni, walikusanyika saa nne, watu wanane, wa kenda Persis Msionaga, aliongezwa siku hiyo hiyo. Hatta Juma a pili ulikuwa Ubatizo saa ya jioni, waliobatizwa ndio watoto watano walioletwa siku hiyo waliovaa nguo nyeupe killa mtu na kofia nyeupe, na killa mtu akapata Mthamini wake aliyekwisha kutiwa mikono, walipokwisha kubatizwa killa mtu alipewa msalaba. Na majina yao ndio haya, Dora na Hermina, wametoka katika "Garnet," Ruth na Adelaide, wametoka katika "Garnet," na Matilda, ametoka katika "Penguin."

Na tena siku hiyo ya Juma a pili jioni saa thenashara lilikuwa kusanyiko la Chama cha Watakatifu wote, ndio waanawake waliokwisha kuolewa, 22; kwanza walifanyiwa chayi na Archdeacon Hodgson, tena walipokwisha kunywa chayi yao, wakaenda kanisani. Tena habari kidogo nitajaribu kueleza, nathani killa mtu atapenda kusikia. Nimempata jamaa yangu mwanamke, nami ndilo jambo nililolitamani siku nyingi tangu kufika inchi hii, na sasa nimekuwa na furaha kwa kumpata, naye ndiye wa kwanza kumwona, lakini ni mtumwa wa watu, nami nimewaomba wapendao kunisayidia, wanisayidie. Baba Archdeacon Hodgson ananisayidia kupata kujua kama nitaweza kumpata.

Lakini naona itafaa zayidi nikianza mwanzo. Tazama, sisi watoto wote tulioweza kwenda tulitoka hapa kwenda kushinda Mwera, na siku yenyewe ndio Jumaa Â'nne Sept. 18, Tulipofika huko Mwera tukapewa chakula ehetu, tukala;

MSIMULIZI 11

tulipokwisha kula, tukatoka kwenda kutembeatembea, wengine tukaenda mtaa mwingine si mbali ya hapo tuliposhinda. Hatta tuliporudi makaoni mwetu watoto wakaanza kucheza, na Wazungu wengine wakaanza kuvua samaki bassi tulipokuwa katika kucheza akatokea mwanamke huyu, alipotokea hakusema neno, lakini alipokaa muda wa saa alianza kucheza na sisi wala hakutuona wageni alituona kama wenzake kabisa, hatimaye aliponiona mimi akanitambua kama mtu wa taifa lake, tukaanza kusema kwa lugha yetu tukaongea kwa furaha, na kuelezana habari za inchi yetu. Tulipokwisha akasema atanifuata aone nyumba ninayokaa, nikamwambia, naona sisi tutafika usiku kwa sababu kwetu ni mbali. Akanijibu hatta mkifika kesho pia lakini nitakufuata, bassi akanifuata hatta hapa petu Mbweni. Bwana na Bibi pia wakaniambia nimkaribishe mezani pamoja nami, bassi nikamkaribisha kwa chakula cha usiku na asubui hatta na cha mchana pia.

Na sasa nitapenda sana awe Mmasihiya kama mimi, nikiweza kumtoa utumwani simtaki kuja hapa karibu yangu kumwona tu, na kufurahi naye, wallakini sababu hupewa ninayomtikia ni kuwa Mmasihiya. Bassi natumaini killa mtu atapenda kusoma maneno haya.

Tena habari kidogo za Waalimu wa Mbweni walioingizwa katika Chama cha Mchungaji mwema ndio kumi na wanne, wameingizwa. July 9, 1885, lakini hawakuingia wote kwa siku moja lakini mwanzo waliingizwa wanane tu na sasa wamezidishwa tena wengine wametawanyika kwanza; Miss Thackeray kaenda Ulaya, tunatumaini atarudi hapa Christmas na tena Lucy na Louisa wamesafiri Chitangali pamoja na waume wao. Louisa anafundisha watoto wa huko, lakini Lucy hatujasikia habari zake kama anafundisha ao siyo, tena Emma ndiye mmoja wa Chama cha Mchungaji mwema pia, alisafiri Misozwe pamoja na mumewe Henry,

MSIMULIZI. 12

na sasa wamerudi hapa kupata hewa, nathani watarudi tena kufanya kazi yao ya kufundisha watoto. Sisi wote tuliposikia kama Emma anarudi tulifurahi lakini tena tulihuzunika kwa sababu walizuiliwa Pangani, ilikuwa vita huko, na vita hii ya Wadoicha na watu wa Pangani hivi hawakuweza kupita, lakini wamefika hapa sasa na killa mtu anafanya kazi yake ya kufundisha watoto, Henry anafundisha Kiungani na Emma anafundisha hapa Mbweni. Na Lydia naye sasa amesafiri bara, nathani anafundisha watoto, naye huyu pia ni mmoja wa Chama chetu, labda anafundisha mahali pa Emma; hatujasikia vema habari zake bado. M.M.

HABARI ZA KIUNGANI.

Katika siku ya Kupriano Mtakatifu Sept: 26 tulifanyiza hapa Kiungani kuwa siku ya Faragha ya rohoni, kwa watu wote wa Chama cha Paolo Mt, waliokuwapo siku ile. Tukaanza Juma a nne jioni faragha yenyewe, hatta Alhamisi asubui. Siku ile tulichojitahidi zayidi kufanya, ndio kujifunza zayidi kwa Bwana wetu, tujitenge kidogo katika mambo ya ulimwengu, tukikumbuka walivyojitenga watu wengi wa zamani, waliomtendea Bwana kazi yake, hatta mwenyewe alitenda hayo. Bassi siku ile ilikuwa ya mafundisho mengi na mema kuwafaa sana wanaotazamia kazi hiyo; tulikuwa naye Kasisi wetu wa hapa, ndiye aliyetwaa kazi hiyo ya kutufundishafundisha, nathani kwanza wote tuliona kuwa ngumu kukaa kimya killa mtu chumbani kwake, illa kanisani, lakini ilipokwisha tukaona imetufaa sana. Siku ya kwanza akatupa fundisho la kutuonya ginsi ya kutumia siku hiyo ya faragha, na kutuonya kama tumhitajie Bwana wetu mno kujifunza kwake, atakuwa ndiye rafiki wa kuongea naye siku ile, na kutuagiza tutumieje wakati wote wa siku ya Faragha.

MSIMULIZI. 13

Assubui ya Juma a tano ulifanywa Usharika Mtakatifu saa ya kwanza, saa ya pili sala ya Assubui na Fundisho, saa tano Litania ya kuwaombea Mataifa na Fundisho, saa a saba, Sext, saa a kumi Litania la Kanisa na Fundisho, saa a pili usiku, Sala ya Alhamisi saa ya kwanza Usharika Mtakatifu na Fundisho la mwisho. Nasi tuliandika Mafundisho haya yote tupate kuyakumbuka. P.L.

Siku hizi Machemba, Mfalme mmoja Myao, aliyeshinda Magwangwara mwaka huu, ametuletea watoto wake watatu wafundishwe, naye anataka kupeleka sita tena waje wakasome hapa Kiungani miaka sita. Naye ataka sana mwalimu Mmasihiya aende akakae mjini pake akawafundishe Anjili. Lakini zamani hakutaka hatta kidogo, sasa anataka sana.

Katika Okt. 4 tulimsafirisha Christopher Kiwapo mwalimu wa Kiungani kwenda Newala kufundisha kule. Amefuatana na Charles W. Rehani, mpishi, aliyemwoa siku hizi Hope Chela, Mbweni. Twasikia wameshuka salama Lindi. Tunatumaini tutaingia Kanisa letu jipya mwezi ukiandama.

Bwana Askofu ameleta simu kusema atafika Unguja Okt. 31. Atapita njia ya Marselz (Marseilles.)

Katika Nov. 26, twamtazamia Mr Travers atafika kukaa hapa Kiungani, na Mr Geldart kwenda Magila.

Habari za Mkunazini.

Norman Namkachapo anapata Ufundi wake katika kazi ya bati mwezi huu, atafanya palepale pa Fundi wake. Luke Walter Kumi, amekwenda kufanya kazi ya upishi kwa Wazungu wageni kule Mvita. Mwezi huu wameanza Sala ya usiku iitwayo "Compline" katika Kanisa la mjini, saa a pili ya usiku.

Sept. 20 walibatizwa watoto watatu wa Miss Mills.

MSIMULIZI. December, 1888. II.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

ANENA MWENYEWE! MSIKIENI!

Mimi ni Msimulizi, ati, ndio jina langu na asili yangu haswa, kwani iko kazi moja ninayoiweza sana, ndio kusimulia ti! Wengine rafiki zangu wataka kuniambia kama jina langu si Kiunguja safi, hunithania labda nimetoka pande za Washenzi, husema Mbona huitwi Msumulizi? kwani sahihi. Lakini, bwana, mimi mzalia wa papahapa Unguja, na ukiuliza Waswahili watupu watakuambia Msimulizi. Wala sitoki ushinzini, la. Tazama joho langu la rangi ya samawati navaa sikuzote, la Kiunguja hili. Hatta huku Unguja pana malidadi, katika kanzu ya bafta hupenda kuchukua alama kubwa ao harufi za jina; kathalika na mimi, bassi. U rathi, bwana.

Bassi nina furaha kama killa upande rafiki zangu wamenipokea kwa furaha, na kuniambia, njoo, rafiki, njoo tena, killa miezi miwili njoo kwetu utusimulie.

Bassi ndio maana nimekuja tena hivi sasa marra ya pili, na safari hii ninakuja burre kama kwanza, unipokee kama zawadi, lakini safari ya tatu utataka kulipa pesa moja, u rathi, bwana, (ao pesa sita kwa mwaka) kwani safari yangu ina gharama, haina buddi.

Bassi kwa killa Mletaji habari yangu nataka kusema Mimi, somo, najua kusimulia tu, ndio maana ukinipelekea maneno ya kusimulia habari za kwako yafaa usichanganye humo maneno ya kuchekeka na mahubiri makubwa ya dini na Majina matakatifu, kwani kuhubiri na kusimulia mbalimbali. Labda pengine nitasitawi hatta nitajua kuchukua mahubiri na mafundisho matupu, lakini kwa hivi sasa ninayoweza sana ni maongo tu, bassi u rathi, somo.

Bassi na killa Mletaji habari alete zile habari za kwake zitakazowapendeza sana watu wa pande zote za Mission. Bassi sasa, bwana, u hali gani? mzima? aaa! mzima, kwani unachekeka, bassi ukae kitako, nikusimulie.

MSIMULIZI 15

HABARI ZA VITA YA PWANI.

Wadoicha wanaona fetheha sana kama mashauri yao yote yamefahitika. Sasa wameshawishi Waingreza huko Ulaya kushariki kazi ya kuzuia na kuwaathibu watu wote wanaochukua watumwa baharini, na wanaochukua bunduki ao baruti. Bassi sasa wanaanza kuvizia pwani yote, Wadoicha wanavizia tangu Tanga hatta kisiwa Mafya na Waingreza tangu Mafya hatta Rovuma, na tangu Tanga hatta Lamu. Merikebu nyingi zinavizia, na merikebu moja kubwa sana za chuma tupu, nene kabisa, inakaa sikuzote bandarini hapa Unguja ina ngome mbili za chuma tupu juu yake, mnamo mizinga ya ajabu mno ya kupigia adui akikaa mbali mayili tano.

SAFARI YA BWANA ASKOFU.

Unguja hatta Mkuzi.

Juma a mosi jioni Nov. 10, tukulala Mkunazini. Bwana Askofu akaniambia nilale chumbani kwake, nipate kumwamsha saa edashara asubui mapema. Bassi hatta asubui ikalia saa ile ya makelele mengi kwani aliiweka ipate kutuamsha kama nikichelewa. Nilipoamka nikamwita Bwana Askofu, kumbe naye alikuwa tayari macho, tena nikaenda kumwamsha Archdeacon Hodgson, kwani alikuwapo. Tukanawa, tulipokwisha saa thenashara tukaingia kanisani. Bwana Askofu akafanya Usharika Mtakatifu katika mathbahu ndogo.

Tulipotoka tukaenda mezani marra moja, tukiisha tukaenda forthani tukaenda pale pa Sayidi tukapakia mizigo, wakatangulia watu wa Mbweni kuuliza kama lini mashua itakuwa tayari.

Na mashua ni ile Chukwani. Walipofika watu wa mashua wakasema, sisi hatuna habari kama tutasafiri, na mashua si tayari, watu wangine hawamo, wala hatuwezi kupakia

MSIMULIZI. 16

mizigo kwani hatta nahotha hayuko, yuko pwani. Bassi Bwana Askofu na Archdeacon wakaingia nyumbani kwa Sayidi kuuliza. Sayidi akasema Ah! nimesahau kumwambia nahotha kusafiri, ngojeni kwanza nitamwambia sasa hivi. Bassi wao wakaenda kwa Balyozi, sisi tukangoja pwani; hatta saa nne wakarudi kutazama, tukaambiwa bado mpaka saa nane itakuwa tayari. Tukaenda kwa Balyozi kungojea, watu wa mashuani wakasema ikiwa tayari tutaleta karibu kwa Balyozi. Waliokwenda kwa Balyozi kungojea ni Bwana Askofu, Archdeacon, Nicholas na mimi; wengine wote wakaingia mashuani kungojea mumohumo, kwani tulikuwa na watu wa Mbweni watano.

Saa saba unusu mashua ikawa tayari wakaila tukaingia. Saa nane kasorobo tukaanza kusafiri. Tukaenda sana hatta kama saa thenashara tukaanza kuona milima ya bara zayidi mlima wa Tungwe kubwa. Kama saa ya kwanza ya usiku tukatia nanga kwani tulikuwa na Waarabu na Nasoro bin Sulemani baba yake Liwali wa Pangani tulikuwa naye na mwanawe mngine jina lake Ali. Yule baba ni mtu tulikuja naye apate kutusayidia Pangani. Yeye ndiye aliyesema tutie nanga, akasema haifai kuingia Pangani usiku tutaumia sana.

Bassi tukalala pale, hatta asubui tukang'oa nanga tukaendelea. Tulipofika milangoni ya Pangani, yule Nasoro bin Sulemani akamwambia Bwana Askofu aingie ndani sana kwani akasema watu wa Pangani wakikuona upesi hawatakubali kuacha kupiga bunduki. Tukaingia Pangani saa nne u robo, tukapigiwa bunduki nyingi nyingi sana hatta Mwarabu mmoja alivaa kilemba ikampiga risasi katika kilemba chake, tena ikampiga ya kiatu msukani karibu kupigwa, nilipokaa dirishani karibu nachungulia zikaja risasi mbili karibu yangu.

Watu wakasema "Amani, Amani," na kuwapungia nguo; kwa shida sana wakaacha kupiga bunduki, na watu

MSIMULIZI. 17

wakashuka upesi kusema kama aliyekuja ni babaye Liwali wenu ndipo wakatulia. Nasoro bin Sulemani akashuka naye na Waarabu wangine wakaenda kuwakusanya madiwani wote wa Abushiri pia, wakawaambia tumekuja na Padre Mwingereza ataka kwenda Magila, je mtampa njia? Abushiri na madiwani wangine wakasema ndio, wangine wakakataa, kwanza wale waliokubali wakaja hatta mashuani pamoja na Abushiri (pangine huitwa Bushiri) na Nasoro, kuonana naye Bwana Askofu, wakasema usishuke leo kwani watu hawajapatana.

Tukashinda pale hatta Juma a nne saa kenda tukashushwa tukapelekwa nyumbani. Balyozi aliwapelekea watu wa Pangani Rs1000 bahashishi wakagawiwa na Nasoro, tena wakaja Waarabu wanaokaa juu kwa Mauya kuangalia habari tuliojia. Nasoro akasema, safari ya Magila Juma a tano assubui, hatta assubui watu wa kutupeleka wakasema si tayari bado, mpaka alasiri, alasiri wakasema, Alhamisi assubui, kumbe zile madiwani wote wamekubali lakini vijana bado hawataki tuende zetu, wataka turudi, ao watufunge, ao wamwue Bwana Askofu. Bassi ile Juma a tano jioni wakaja vijana wasita wakasema twamtaka Mzungu tuseme naye, na mlangoni petu wamewekwa viroboto wanane kungojea mlango hawamwachi hatta mtu mmoja kupanda juu, illa Bwana Askofu asema mwaachieni; wale wakapewa ruhusa wakaja hatta juu, maneno yao wakasema Twataka utupe kitu kama fetha tukatumie, Bwana Askofu akawaambia Siwezi kuwapeni fetha wala chochote, kwani nikiwapa ninyi killa mtu atataka. Wakatoka wakaenda zao, wakakusanya wenzao wakafanya mashauri kama tuwangojee njiani tuwapige tunyang'anye mizigo, shauri lile likasikiwa nasi na madiwani pia na Waarabu.

Assubui ikawa uthia sana, vijana wote wanataka kuchoma mji waende zao mbali. Tulikuja na mtu mmoja Wa Pangani kutoka Unguja yeye ndiye mfitini sana, hujifanya

MSIMULIZI. 18

mwema huku na huku huwaambia wenziwe, Msimwache Mzungu kupita, illa atoe mali, mtu wenyewe jina lake Shomali. Abushiri akasikia wafanyavyo hawa vijana, na Nasoro akasema na Bwana Askofu heri turudi, lakini Abushiri akasema Nimeahidi kwa Balyozi Mwingereza bassi siwezi kuvunja ahadi yangu, nitampeleka huyu hatta atakako, na nitawashusha wale atakao washuke. Akawaendea wale vijana waliokwenda kutungoja akawatukana sana akawaambia Mkimpiga huyu, mwagomba na Sayidi Khalifa, akasema Mimi nitampeleka hatta Magila, na atakaye vita na aje kwangu, akapigiwa bunduki tatu hazikulia naye ana upanga tu, akampiga mtu mmoja kofi. Akarudi, marra alipopita kidogo nyumba yetu, tukaona jeshi lao vijana wote kama watu thelatha mia wakaizunguka nyumba wakataka kuingia ndani kutukamata. Marra viroboto waliokuwa wakitungojea wakajiweka tayari kwa kupigana, na Abushiri na Mwarabu mwingine jina lake Muhammadi bin Azizi wakarudi upesi mlangoni hawana bunduki illa panga tu wakazitoa wakaanza kuwafukuza watu wale wote, na yule Nasoro bin Sulemani akapata habari akaja na Waarabu wengi wakataka kupigana, ikawa uthia mwingi sana, baadaye Nasoro akanwambia Bwana Askofu heri kwenda nami kwangu, Askofu akasema haithuru nitakaa papa hapa, sioni hofu, tena Nasoro akasema tungoje mashua itiwe moto turudi Unguja. Abushiri akasema ni aibu tukimrudisha pasipo kumpeleka Magila, itakuwa kama tumeshindwa na hawa vijana. Majumbfe wangine wakawakamata vijana vyao wakatiwa gerezani kwa siku moja. Tena Nasoro akatoa Rs 500 akiwagawia.

Jumaa Nov. 16 Abushiri na madiwani watano, na Ali bin Nasoro, na Waarabu wangine na vijana wangine, wakaingia safarini kutuleta hatta Mkuzi. Tulipofika Kakindu tukakaa sana tukapika chai, nao wakapika chakula chao.

Tulipofika Mkuzi wakapewa ng'ombe na mbuzi kitoweo

MSIMULIZI. 19

chao. Tukamkuta Bwana Goodyear, naye akaenda upesi Magila kuwaambia mabibi washuke, wakaja usiku kwa usiku, naona hawakupenda hatta kidogo kushuka. Assubui Juma a mosi wakaja Pangani, vijana watatu walirudi nyuma kwa matisho wakasema wataka kitu tena, ao watawathuru mabibi, lakini hawakupewa chochote. P.L.

HABARI ZA MBWENI ZA ZAMANI.

Zamani Mbweni ulikuwa mji mdogo sana. Ilikuwa nyumba moja tu ya mawe, nayo ndogo, ina vyumba vitatu, viwili chini na kimoja juu, viwili vya chini ndio ile sebule sana na ile ghala, na madaraja yake kwenda juu mabovumabowu hatta huwezi kwenda juu ila kwa kutambaa. Na msimamizi aliyekuwapo wakati huo Wadi Hamisi, na Hamadi, na Farahani, chini yake, na Ali Mtanga karani wake. Na juu ya Wadi Hamisi Bwana Mr. Morton. Tena wakaanza jengo, kwanza wakajenga uwa, na watoto wakilala uwani popote chini, zamani hizo hapana vitanda, wala mikeka miwili wala nguo ya kulalia wala ya kujifunika wala hapana starehe kama sasa. Na Bibi aliyekuwako zamani hizo, ah, siwezi kusema, kwani nitawakasiri wengi. Na katika habari za chakula, siwezi kutaja meza, kwani hatta hiyo killa mtu kupata sahani yake hayakuwapo, zilikuwapo sahani sita ao saba ao tisa za wakubwa, na wadogo palikuwa na mabakuli makubwa matatu, bassi humo hutiwa wali na mchuzi na nyama, haya tena wakapewa wadogo, bakuli watu wanne ao watano ao sita, haya tena hunyang'anyia, aliye mnyonge siku hukosa, basi hivi walio wadogo wakathii. Na tena kusema kama palikuwa na kushukuru mbele ya chakula ao baadaye sina hakika. Na juu ya haya yote watoto wakapata furaha. Na baada ya chakula cha athuuri, watoto wanakwenda kuoga na kucheza sana majini mpaka saa nane kengele ipigwe kwenda kusoma, na jioni watoto hucheza sana na mchezo wao ndio msoma,

MSIMULIZI. 20

hucheza mpaka saa tatu ya usiku huenda kulala. Tena hapakuwa Kasisi hapa, toka Mbweni hatta Kiungani hatta Mjini, Kasisi mmoja tu. Bassi ilikuwa killa Juma a pili hutoka watu kwenda Kiungani ao Mjini kwa Usharika na Sala. Ao Juma a pili ingine huja yeye Kasisi huku. Na habari za shamba hili halikuwa kubwa kwanza, mpaka wake ulikuwa ile barabara ya bandani na mchungwani na hatta barabara ya Kanisa lile kubwa bassi. Toka bandani hatta kisima cha bomba ndio shamba la Mwarabu jina lake Binti Bushiri. Na huku upande wa pwani ndio la Mwarabu mgine jina lake Ali bin Isa, na hili la Balyozi sasa lilikuwa la watu watatu, wa kwanza Selemani Marhubi, wa pili Binti Saadi Masidi, wa tatu Alfani bin Amri, hawa ndio majirani yetu wa karibu. Na zamani hizo hapana barabara katika shamba kama hizi sasa, pale palipo nyumba ya Mwalimu palikuwa nyumba ya udongo, na baadaye kidogo palikuwa nyumba ya msimamizi, na mbele yake kidogo panapo nyumba ya serikali ya kina mama wakubwa ya udongo, ilikuwa nyumba ya msimamizi mdogo aliyeitwa Farahani. Na baadaye ukirudi nyuma kidogo panapo kisima eha mkuyu palikuwa na nyumba ya msimamizi Hamadi, na mbele yake kidogo palikuwa nyumba mbili tatu za wajoli. Na yule msimamizi Hamadi ndiye hushika posho ao chakula cha wajoli. Na kazi ya wajoli kulima, na miwa mingi ilikuwapo na hii miwa ikashindikwa asali, lakini haikushindikwa hapa ilikuwa ikichukuliwa. Maungani ao Langoni, ndiko kwao yule msimamizi nako ndiko kunako hicho kinu cha miwa; asali nyingi ilikuwapo wakati huo, nusu ikatumiwa nyumbani na nusu ikauzwa. Na wajoli hufanya kazi mchana kutwa jioni hupokea fungu moja la mhogo na pesa moja killa mtu mke kwa mume vivyohivyo isipokuwa Juma a mosi ndio fungu la mhogo na pesa mbili na kibaba cha mtama. Na nyumba moja walikaa watu wawili ao watatu killa

MSIMULIZI. 21

mtu na mkewe. Hapakuwa killa mtu na nyumba yake kama sasa ao kutwa pesa kumi ao asharini kama sasa, la. K.M.

KULIZINDIKA KANISA LETU LA KIUNGANI.

Katika siku ya Juma a nne Nov. 6 ndipo tulipolizindika kanisa letu. Kwanza wageni wa Mbweni na Mkunazini walikuja assubui saa ya thenashara unusu ya assubui, hatta saa ya kwanza kengele zikapigwa, na waimbaji wakavaa nguo zao na watu wote tukaingia kwa sala ya kwanza ilio kuu, na wangoje na waimbaji wakalizunguka kwa ndani na watu wote wakiimba na uvumba ukivukizwa, kiisha wangoje na waimbaji wakarudi mahali pao, ndipo ikaanza sala yenyewe, na Askofu ndiye aliyefanya, tena sala ikaisha. Tangu assubui hatta jioni ikawa kucheza na kufurahi tu. Saa a sita ndipo watoto wote wa Kiungani na Mkunazini na Mbweni tukapewa chakula chetu cha mchana; kiisha Wazungu wakaenda mezani saa saba, na siku hiyo Wazungu wengi walikuja. Saa kenda u nusu hatta saa edashara wakazidi kuja Wazungu wangine wa mjini na wa merikebu, ni kuja kulitazama. Mwisho saa edashara za jioni killa mtu akarudi kwake.

Jioni palikuwa sala kubwa ya jioni ya kushangilia, na Mr. Jones-Bateman akatoa khutuba, kiisha sala ikaendelea, na marra ya pili wangoje na waimbaji wakalizunguka ndani na watu wote wakiimba na uvumba ukivukizwa, tena sala ikaisha; tena pakawa na machezo tu mpaka saa nne ya usiku, bassi. Mtg.

HABARI ZA BOONDE.

Magiza, Nov. 11,

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu, ya kwamba mwezi huu tulikuwa na shaka sana ya meli kwa ginsi ilivyokawa kufika hapa hatta

MSIMULIZI. 22

hatukujua iliyoipata, illakini ilipowasili tukajua sababu yake, ya kwanza, twasikia kwamba vyombo shidda kukubali kutoka Unguja kuja Pangani kwa ginsi vinyavyopata taabu nyingi vikikaribia bandarini, kwani watu husimama pwani mchana na usiku na bunduki mkononi, tayari kungoja itakayoupata mji wao, kwa ajili hiyo killa chombo kijacho Pangani kikikaribia milangoni hupigiwa bunduki zenye risasi hatta kitue kuko huko njiani, kikiisha tua huwauliza watoka wapi na, nani abiria waliomo ndani? Ikiwa hamna Mzungu huambiwa, haya tweekeni mwingie bandarini, na sababu ya pili meli ikakawa kwa kuwa pepo za mbisho wamekaa siku nne baharini, napo ni mahali pa siku moja tu kufika Pangani ao Unguja.

Kwenyi Jumaa Nov. 9 baada ya kufika Meli kama jana, hatta Jumaa alasiri saa edashara tulipotoka Chuoni Darasa ya waalimu, Mr. Goodyear akatuita chumbani kwake waalimu wote kadiri tulivyo hapa; tulipofika kwake, awali akatutolea vyuo vya Vita ya Rohoni, na baada ya hiyo akatutolea Msimulizi, naye Msimulizi huyu akaupendeza sana kwa mashauri aliyo nayo na kazi atakayotenda, twaona atafariji wengi, kwa hiyo tulipendezwa sana hatta tukamchagua mwalimu mmoja papo kwa papo awe Mletaji habari, na watu wengine hawakuweza kupewa habari siku hiyohiyo kwani ilikuwa jua limetua kabisa. Wakaku anywa kwenyi Juma a pili Nov. 11 saa tano wapate nao wajue habari ya Msimulizi, nao wakapendezwa sana kwa shauri hili, wallakini twaona safari hii haitapatikana habari nyingi kwani ni jambo la ghafula twatumaini kama habari hii ikizidi kuzoea na maneno yatazidi kuwa mengi, kwa hiyo twataka mzidi kuwa rathi sana.

Tena tazama tofauti iliyo mioyoni mwa Wabondei kwa dini yetu ya Kimasihiya.

Baada ya siku kuu ya Watakatifu wote, nilikwenda

MSIMULIZI. 23

kutembea mjini mwa Wabondei nikakutana na Jumbe mmoja wa Kibondei, tukaamkiana tukaisha, baada ya kuamkiana, nikamwuliza mbona siku hizi sikuoni kanisani? Akajibu, akanena, tangu umekwenda Unguja sikuacha kwenda kanisani isipokuwa juma hizi mbili tatu ndio sikuja kwa uthuru nilio nao, hamjibu Ndio, lakini uthuru wa dunia si kama uthuru wa roho, akanena, Ah, kweli, lakini hatta tukija kusali fayida yetu nini? Nikamwambia utaokoa roho, na zayidi ya hiyo huna buddi kumtumikia Muumba wako, akanena ndio maneno yenu mazuri lakini mbona hayaonekani mnenayo? Watu wa pwani wakisema neno sharti utaona vilevile. Hamwaambia Ndio, walakini mwajua kama watu wa pwani wataka mali yenu tu, wapoteze roho zenu kwa hirizi zao, na kwetu mtaokoa roho siku ile kuu wafu watakaporudi tena. Nilipomtajia ufufuo akashangaa mno akanena hayo ni maongezi mazuri ya kusikia, lakini ni hadithi tu hizo.

Nami hujaribu kumwonyesha nguvu na upendo wa Muungu kwa kutuumba na mwisho atatufufua, kwa maneno kama haya; akaamini kidogo si sana, natumaini mwisho wa yote ataamini sana. A.M.

NJAA, KIU, HATARI, KUPOTEA.

Nov. 30 ilikuwa siku kuu ya Andrea na ya kanisa letu kwa jina lake Andrea, tukacheza kutwa, hatta alasiri yapata kama saa nane tukaenda pwani kuchezea ngalawa, zilikuwapo mbili, moja tukachezea sisi wangine, na Cyprian Lizani na Mr Bone, wakatweka tanga wakataka kwenda Mbweni tanga, likawashinda wakalitua kiisha wakatumia kafi mpaka Mbweni, tukathani watarudi jioni, jioni tukangojea wasije, kengele ya jioni ya kwenda kusali ikapigwa, tukaitwa majina hawajaja bado, tukangoja hatta saa tatu tukatuma watu wawili Philip Yahom na Yakobo Chorola Mbweni tusiwapate. Saa tano usiku akaenda Mr Watson na

MSIMULIZI. 24

Peter Selenge na Herbert Feruzi, kunako H.M.S. Boadicea, Mr Watson akaingia mnamo mashua ya moshi kwenda kuwatafuta mpaka Chumbe usiku kucha wasiwapate, mpaka asubui wakarudi, tena Mr Highton akaingia ndani ya ngalawa akaenda usiku kucha huko na huko mpaka Chumbe asiwapate tena.

Juma a mosi Admeli akapeleka mashua mbili, na Mr Clarke akapeleka vyombo vitatu, na Mr Wallis akapeleka dau moja la mvua samaki kwenda killa mahali kutafuta habari zao akipata atapewa Rs 60, lakini wapi, wasipatikane, Juma a pili Balyozi akapeleka mashua 20, Agamemnon, alipeleka mashua iendayo upesi sana yaitwa "torpedo boat" kwenda kuwatafuta mpaka Bagamoyo, lakini yote burre, na sisi tukaweka taa madirishani mwetu wapate kuziona, lakini wapi; tukazidi kuwa na mashaka sana kama wamezama ao wamekufa kwa njaa na kiu, kwani hamna chakula wala maji mwenyi ngalawa; tukawa tukiwaombea marra kwa marra kanisani, kumbe Juma a tatu saa thenashara bado walitokea Kiungani. Na habari zao ametuandikia Cyprian hivi:

"Saa nane unusu mimi na Mr Bone tukaingia katika ngalawa kwenda Mbweni tukafika. Mr Bone, akashuka kwenda nyumbani kuitazama Mr Highton lakini hakumwona; na mimi nikashuka pwani kutembea kidogo, na ile ngalawa imekokotwa kidogo hatta ikiwa na nanga, Mr Bone akaja, wote sisi wawili tukaingia, tukatweka tanga kuja zetu Kiungani, lakini tulianza kwenda njia ya chini tukachukuliwa na maji hatta kwenyi fungu la mchanga lile lililo karibu na Bawe, usiku tukafika funguni. Tena tukatweka tanga tukaenda kwa kushuka upande wa chini, kusini, tukaona tanga halifia kabisa tukatua, tukajaribu kwenda kwa kafi hatukuweza tukazidi kukokotwa na maji nasi tumechoka. Lakini tukatweka tena na kuvuta kafi tusiweze tukaacha tu, na tulipoamka asubuhi siku ya Juma a mosi

MSIMULIZI. 25

tukaona huko mbali karibu sana na kisiwa Chumbe, pale karibu na kisiwa Chumbe tukatweka tupate kushuka pale kisiwani, marra upepo ukaja ukatukokota tusiweze hatta kidogo kushuka Chumbe, tukataka kutia nanga, lakini jiwe dogo na kamba fupi, tukavuta kidogokidogo tu; Marra tukaona manowari ya Mdoicha ikipita karibu yetu ikienda njia ya kusini tukaita itusayidie lakini haikuja ikaenda zake tukaona mtumbwi ukivua tukauita uje kutusayidia wenyewe wakasema tutakuja lakini hawakuja wakaenda zao tu. Na wakati huo sisi tulitweka tanga kaskazi ikavuma sana pamoja na mvua, ngalawa yetu ikazidi kwenda upesiupesi mwenyi Mwamba-ukombi na Kwale kwa chini tukakiona, tulipokaribia huko tukatua tanga tukajaribu kuvuta kafi hatukuweza kwani tukachoka na kafi moja ikapotea. Tukawa wote tumekaa kwani hatuwezi kufanya lolote, na katikati ya bahari tukikokotwa tu, tukaviita vyombo vingine vingine havikuja, tukatia alama nyeupe juu ya mlingoti lakini hapana kitu cha kutusayidia usiku tukalala wote na mawimbi yale makubwa yakitukokotea upande wa kusini wa Bagamoyo kidogo.

Bassi ikawa assubuhi; ndiyo Juma a pili ya Kuja kwake Bwana wetu, tukitazama huko na huko Unguja hatukuiona tena, illa tukaona Afrika mbele yetu, tukasema, twende Afrika tukipona vyema tukifa bassi. Tukatweka tanga tukaenda rahisi sana kwani kushuka si vigumu, lakini msukani umevunjika kwani Mr Bone alianguka majini, ikawa kusayidiana tu, kutwa tukawa baharini, tukaona karibu kufika pwani, tukaona ngalawa kubwa tukaiita ikaja karibu nami nikasema tupelekeni Unguja nitawalipa mali, wakasema shukeni pwani kwanza, lakini hawakuja. Tulipoanza kushuka nikamwambia; Mr Bone wewe kaa nyuma akakaa, mimi nikawa mbele ikiwa hatari, inipate mimi kwanza.

Naswi tukashuka sisi wote wawili, naye Mr Bone hajui Kiswahili bado; nikamwambia usiseme neno mimi nitasema

MSIMULIZI. 26

na ngalawa tumeitia nanga, na tulipokuwa tukienda nikamwambia kaa nyuma, lakini nikaona haifai kwani hatari ikiwa sitajua, nikamwambia aende mbele, bassi yeye hakupenda kupita mchangani kufika penyi mji mmoja ulioko karibu na pwani pale, akapita njia za vichakani, na marra bunduki moja ikapigwa akastuka, tena akarudi katika njia zile. Nikawauliza watu huku hapana Mhindi? tukaambiwa hapana, nikauliza wala Banyani hapana? nikajibiwa yupo, nikamwita mtu mmoja tangulia utupeleke kwa huyo Banyani, tukaenda hatta tukafika, marra watu wakapata habari kule mjini kama Mdoicha ameingia, Waarabu na Waswahili wengi wakaja kumtazama, wengine wakataka kumpiga bunduki, bassi mimi nikaona ndiyo mwisho wangu wa kufa, bassi mimi nikafanya bidii kumsayidia husimama mbele yake wapigao wanipige mimi, marra tatu nimemzuia kama kupigwa ningekufa mbele kwa ajili yake huyu Mr Bone, bassi Waarabu kwa ukali wao, naliinama chini nikaomba nife katika amani, nisitetemeke. Nikawajibu kama huyu ni Mwingereza wala siyo Mdoicha, nikashindana nao sana, mwisho nikawaambia tazameni nguo zangu kwani za Kiingereza, tena wengine wakasema kweli ndiyo Mwingereza tukaachwa kwa shidda sana, tena akawekwa ndani nyumbani mwa Banyani. Tumefika saa sita kwake huyu Banyani.

Lakini watu watatu wakataka kumpiga bunduki tena ikawa amani kidogo, tukafanyiziwa chakula wali na embe tatu pia kwa haraka tukala killa mtu na sahani yake Mr Bone ndani na maziwa pia akapewa. Tulipokwisha kula, akaja mwenyewe Jumbe Dilunga jina lake, aliye chini yake Muhammed Bin Useni, mwanawe jina lake Mikambi. Mji jina lake Kiumba Wageni maana yake Jumbe apenda wageni. Zamani mahali hapo paliitwa Ukutani. Baada ya haya uthia vile vile, hima watu waende

MSIMULIZI. 27

zao Unguja, bassi Jumbe Dilunga akatupa ruksa ya kurudi. Naye akasema nitakupa mtu wangu mmoja awarudishe lakini mimi nataka unipe zawadi ukifika huko Unguja kama ukipewa mpe huyo Wadi Shomili alete, kama hakupata bassi, tukapatana kwa rupia nane. Tukamwaga yule Banyani na watu wengine pia na wengine walinitambua mimi pia kidogo tu. Tulipofika pwani watu wengine wabaya wakavuta visu vyao labuda wataka kumpiga Mr Bone, na ngalawa kubwa ikawa tayari kuingia, mimi nikamwambia ingia upesi wewe kwanza, mimi nikangoja, akaingia upesi ndani ya ngalawa, na mimi ndipo tena nikaingia, lakini watu wengi hawakupenda nirudi huku Unguja, bassi Wadi Shomali (jina la mtu aliyetuleta) akatweka tanga lakini upepo hapana, tukaenda kwa kafi, hatta baharini ukaja upepo kidogo tukaanza kwenda hima upesi kwa upepo mzuri sana, na ile ngalawa ya Mr Bone, nikamkabithi huyo Wadi Shomali nikamwambia lete nitakupa Rupia tatu akajibu vyema.

Bassi na ngalawa hiyo ilikuwa ikienda upesi sana, marra tatu ikataka kupinduka kwa kwenda upesi mno, tukaanza kuona Kwale kwa njia ya chini wakati wa kurudi, tukapita na kisiwa Mwamba-ukombi, ndiyo iliyo karibu na Chukwani lakini usiku, tukatua tanga tukaenda kwa kafi usiku kwa usiku hatta kupita Chukwani kidogo, tukakaribia pwani karibu na assubuhi ndipo tena tukashuka tukapita njia kuu, na Wadi Shomali tunakwenda naye, tukamwambia tufuate hatta kwetu Kiungani tukafika kwetu assubuhi saa thenashara, ndugu wakafurahiwa sana walipotuona sisi wote salama tumerudi."

Bassi Juma a tatu walipoletwa na mtu yule katika ngalawa siku hiyo Mission zote tatu, Mbweni, Kiungani, Mkunazini hawakusoma, huwafurahia ndugu zetu, na kushukuru kwani haja zetu zimetimizwa.

MSIMULIZI. 28

HABARI ZA MKUNAZINI.

Michael Chake ametoroka yeye na Jude Mchahowia, wamekwenda Kongo. Na Luke Mabruki amekuja kukaa huku. Na Ijumaa siku hizi inakuwa mahubiri kwa Waislamu wengine waliokuja kusikiliza na aliyehubiri ni Mr. Clarke na wengine.

Na tena Meli hii amekuja Mzungu mmoja anakaa kwetu jina lake Mr. Combe, kazi yake kutazama chakula chetu.

Na Mr. Maxwell na Mr. Coggan wamekwenda zao Ulaya. G.D.

Habari nyingine za Kiungani.

Oct. 26, alikuja Bwana Askofu na Mr. Geldart, akafika hapa Kiungani saa tissa urobo, tukatoka chuoni hatukuingia ten i tukaenda mwamkia sebuleni.

Nov. 8 Tulifiwa na ndugu yetu mmoja Luke Idi. Alikufa kwa ugonjwa wa kitwa akiagua siku mbili tu. R I.P, (Requiescat In Pace, maana yake, astarehe katika amani.)

Nov. 12, alisafiri Bwana Askofu, akamchukua naye Peter Limo. Balyozi alimzuia Mr. Geldart asiende, bassi yupo hapa siku hizi akitufundisha.

Samuel Sehoza ameingia Chama cha Paolo Mt. mwezi wa November.

Swithun Ulumana amepolekwa kukaa kwa watoto wa kazi Mkunazini, anajifunza kazi ya sermalu.

Samwil Chiponde amepewa ualimu kwetu siku hizi.

HABARI ZA MBWENI.

Archdeacon Hodgson alisafiri Nov. 20 kwenda Ulaya. Mr. Wallis na Mr. Hainsworth sasa wapo Mbweni. Miss Thackaray anatazamiwa mwezi huu.

HABARI ZA NYASSA.

Tulisikia kama Mr. Johnson aliandikia Oktober, jahazi Charles Jansen imekwama katika Shire karibu na Malombe kwa kusini. Denys na W. E. Kanyopolea

MSIMULIZI. 29

wamemfikia wameanza kazi ya kufundisha palepale, na Augustin na Aruffo na wake wao wapo Matope wakifundisha kule. Wanangoja maji yajae labda mwezi wa December, waende zao Lukoma. Na Archdeacon Maples anasema kama kule Lukoma pana watoto 57 wanalala nyumbani na wanafundishwa na Murphy Makamla. Na waanawake wengi siku hizi wamefanywa waanafunzi.

HABARI ZA NEWALA.

Tumesikia, inapopigwa chapa Msimulizi hii, yakuwa wamepatwa na huzuni sana kule Newala; Stefano Kalewa alicheza na mtoto mmoja mwenzake aliyeshika bunduki imetiwa marisawa, akaipiga kwa bahati akampiga Stefano akafa palepale upesi Nov. 13, R.I.P.

Tumepokea barua mbili ndefu katika waletaji habari wa Mbweni lakini hapana nafasi ya kuziingiza humo.

Tunataka kuletewa majina wa Waletaji habari ya killa mahali na ya watu wote watakao Msimulizi killa miezi miwili. Meli hiyohiyo tunataka yasikawie. Mtg.

Na wapiga chapa hapa wanasema tumwambie killa Mletaji habari aandike maneno yake katika upande mmoja tu wa karatasi zake, na upande wa nyuma auache mtupu.